



Roma, Machi 25, 2021
Sherehe ya Kupashwa Habari ya Kuzaliwa Bwana

Mwaka wa shukrani kwa Mwenyeheri Francis Jordan

2021 – 21 Julai – 2022

Wapendwa Masista, Wanashirika, na Wanafamilia ya Kisalvatorian,

Kwenye Sherehe hii ya Kupashwa Habari ya Kuzaliwa Bwana, tunawasalimu kwa mioyo yetu iliyojaa furaha, shukrani na matumaini. Tunawaandikia barua hii katika majuma yanayotangulia sikukuu ya Kutangazwa Mwenyeheri kwa Mwanzishi wetu, Pd. Francis Jordan. Ni wazi kwamba hii ni sherehe ya Kanisa lote ambayo inapita zaidi ya upeo wa Familia yetu ya Kisalvatorian. Ni utambuzi wa ushuhuda wa utakatifu wa kitume kwa watu wote wa Mungu walio safarini. Walakini, hatuwezi kukataa kwamba maisha ya Mwanzishi wetu na kutangazwa kwake Mwenyeheri, kwetu ni tukio la Roho wa Mungu ambalo limekuwa njia ya maisha na utume.



Kwa kuzingatia mazingira haya ya sherehe na kama njia ya kutoa shukrani kwa ushuhuda wa utakatifu wa kitume wa Baba yetu wa kiroho, tunapenda kutangaza **“Mwaka wa Shukrani kwa Mwenyeheri Francis Jordan”** ambao tutauanza Julai 21, 2021 na kuendelea hadi Julai 21, 2022. Utakuwa wakati wa neema kwa Wasalvatorian wa kila kizazi, hali za maisha na tamaduni. Tunawaalika ninyi nyote kuungana katika mipango anuwai ambayo itatuongoza kuimarisha wito wetu wa kitume wa thamani, kuimarisha uhusiano wetu wa ushirikiano muhimu na kuhuisha huduma yetu nyenyekevu ya kimisionari lakini thabiti katika Kanisa.

Na tusherehekee mwaka huu maalum kwa furaha na kwa kina, kama wana na mabinti wa kiroho wa Pd. Francis Jordan. Na tuwe wabunifu na kufanya mipango madhubuti na halisi ya utajiri wetu wa kitamaduni na halisia tofauti. Tunawaalika kuwa tayari kwa kiwango cha juu, kuandaa mpango wa pamoja kama Familia ya Kisalvatorian, tukijua kuwa kwa njia hii tutaaheshimu msukumo anzishi wa Padre Francis Jordan. Kutangazwa kwake mwenyeheri ni chanzo kipya cha msukumo na hatua ya uongofu kwa kiwango cha kibinafsi, kijumuiya, na

kitume, ili isiwe kumbukumbu rahisi, bali *kairos* (mang'amuzi ya wasaa) ambayo yanatuwezesha kuwa *koinonia* (washirika na Mungu na Wakristo wenzetu).

Mwaka huu wa Shukrani na uwe wakati wa baraka kwa Familia nzima ya Kisalvatorian na katika mazingira tofauti kabisa! Ili kufikia vizuri sana mwisho huu, tumeunda "Tume ya Pamoja ya Kimataifa ya Utambulisho na Utume wa Kisalvatorian" kutusaidia kusherehekea kwa harambee mpya na ya ubunifu kati ya wote, ikitupatia nyenzo muhimu. Kwenye kurasa zetu za tovuti kutakuwa na kiunga juu ya "*Mwaka wa Shukrani kwa Mwenyeheri Francis Jordan*" kuanzia juni 16. Katika tovuti hii dhahiri utapata, kwa lugha tofauti, mapendekezo ya sala, picha, shughuli na maadhimisho. Tunatumia fursa hii kuwaalika kututumia rasilimali zilizotengenezwa katika Vizio vyenu na ambazo mngependa kushirikisha ili zipatikane kwa Familia nzima ya Wasalvatorian. Umoja ni nguvu!

Kwa kuongezea, juu ya mipango hii yote kwa pamoja, ni matakwa yetu kwamba Kutangazwa mwenyeheri kwa Mwanzishi wetu kusiwe tu ni mfululizo wa "jitihada za nje", za kijumuiya au za kiasasi, lakini pia hafla ya mambo ya ndani, ambayo huenda ndani na kwa uhakika, kama wito kwa wote kuishi wito wetu kwa utakatifu. Kwa kuongozwa na ushuhuda wa utakatifu wa Mwanzishi wetu, na tupate kufanikiwa kuwa "*mitume nje ya mipaka*", kwa maisha yenye kuzaa matunda, ubunifu na mwelekeo wa juu, kama vile yeye mwenyewe alivyopendekeza kwetu: "*Iweni watu wa sala na mtafanya mambo makuu.*"

Tunatanguliza shukrani kwenu kwa mambo yote mazuri ambayo mtafanya katika mwaka wote huu wa sherehe, mkiipa uhai karama ya kitume ya Mwenyeheri Francis Jordan. Kupitia ushirikiano huu kati yetu sote, karama hukua na kutoa matunda katika hali tofauti za ulimwengu. Tunawahakikishia sala zetu, tukimwomba Roho Mtakatifu kutujaza, kutuongoza na kutuangazia katika njia hii. Huu ni wito wetu wa pamoja: kuwa mitume wa Yesu Kristo kila mahali kwa bidii kama ile iliyokuwa kwenye moyo wa kimishonari wa Mwenyeheri Francis Jordan!

Katika umoja wa furaha,



Pd. Milton Zonta
Mkuu wa Shirika SDS



Sr. María Yaneth Moreno R.
Mkuu wa Shirika SorDS



Bw. Christian Patzl
Mratibu Mkuu ICDS